**336/2**
**Lugha ya**
**Kiswahili**
**Paper 2**
**2Hours**

# MEPSA RESOURCEFUL ASSESSMENT 2024

Uganda Certificate of Education

LUGHA YA KISWAHILI 336/2

UFAHAMU NA FASIHI

**MUDA : SAA MBILI**

**MAAGIZO;**

- Jibu maswali **Mawili .**
- Jibu maswali yote katika sehemu **A** na sehemu **B**.
- Maswali yote ni yalazima kwa wote.

***Pindua***

## SEHEMU A: UFAHAMU.

1. **Soma makala Kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;**

Kwa muda mrefu, nchi ya Uganda imekumbwa na majanga mbalimbali katika sehemu nyingi za nchi. Majanga haya mkiwemo; njaa na ukame huko karamoja, mafuriko katika sehemu za Teso, maporomoko ya ardhi huko Bududa, mtetemeko wa ardhi katika kaunti ya Kakuuto wilayani Kyotera, radi kali huko Mubende na uvamizi wa nzige huko Karamoja.

Miaka miwili hivi nyuma, dunia nzima ilishuhudia janga la kimataifa la ugonjwa wa UVIKO19. Kirefu cha UVIKO ni Ugonjwa wa Virusi vya Korona. Chimbuko la virusi vya ugonjwa huu sugu linaaminika kuwa nchini Uchina katika mji wa Wuhan. Virusi hivi vilizuka mnamo mwezi Desemba mwaka 2019. Ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na virusi ya Korona. Virusi hivi ni vipya duniani. Ni maafa makubwa katika historia ya dunia nzima**.** Ugonjwa huu ulivunja rekodi ya kimataifa ya kuua mamilioni na mamilioni ya watu duniani ndani ya muda mfupi!

Wanasayansi wanasema kwamba Ugonjwa huu wa UVIKO19 unasambazwa kupitia njia ya kupumua na kuvuta hewa yenye virusi vya korona, njia ya kushikana mikono, kubusu na kugusa mwili wa mgonjwa aliyeugua ugonjwa huu, njia ya kushika uchafu au vitu maji maji vya mgonjwa wa UVIKO19, njia ya kunywea kwenye chupa au kikombe kilichotumiwa na mgonjwa.

Dalili za ugonjwa huu wa UVIKO19 ni Kama kuumwa macho, kichwa na sehemu nyingine za mwili, kuugua homa, kukohoa na kupiga chafya, joto la mwili kupanda sana. Ugonjwa huu ulisambaa katika dunia nzima kwa mwendo wa kasi sana hadi nchi kubwa Kama vile; Marekani, Uhindi na nchi nyingi za Ulaya kama; Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Ugiriki na Urusi. Dunia nzima ilijaa huzuni na hangaiko! Nchi tajiri na maskini zilifunga shughuli na biashara nyingi za kitaifa na kimataifa kwa muda fulani. Vifo vya watu vilipoongezeka sana, nchi zote ziliamua kufunga usafiri wa angani, barabarani, majini pamoja na mipaka yote kufungwa.

Rais wa nchi ya Uganda Katika hotuba yake aliwaambia wananchi kujihadhari na janga la Korona. Rais alipendekeza njia kadhaa za kujilinda dhidi ya ugonjwa huu wa UVIKO19 Kama Kutoshikana mikono, kukaa nyumbani, kunawa mikono
Kwa maji na sabuni, kutumia sanitaiza, kuacha nafasi ya urefu wa mita mbili Kati yako na watu wengine, tusikohoe ovyo ovyo hadharani, kutoshiriki mapenzi na wageni, wahutumiwa na waathirika wa virusi vya korona kuwekwa karantini na kutoa matibabu mwafaka kwa wagonjwa wa UVIKO19.

Maelfu na maelfu ya watu walikuwa wakiaga dunia kila saa na dakika. Takwimu rasmi za shirika la umoja wa mataifa (UN) zinaonesha kwamba, watu milioni 7 walifariki dunia kutokana na UVIKO-19, lakini idadi ya kweli inaweza kufikia vifo vya watu milioni 20. Hii ni kwa sababu nchi nyingi hazikuhesabu vizuri vifo vya Korona. Sehemu za kuabudia ikiwemo makanisa, mahekalu, matambiko na misikiti yote ikafungwa. Watu waliishi kwa hofu kubwa na wengine kutamauka kutokana vifo vya halaiki. Kwa mara ya kwanza, watu walijifungia ndani kwa ndani majumbani kwao. Waathirika wakafungiwa karantini kama wafungwa gerezani. Nyuso nzuri za warembo, wazuri na wabaya zikafunikwa kwa maski au mabarakoa! Maski zikawa bidhaa muhimu, kinga na mwokozi wa maisha katika kipindi cha Korona.

**Maswali;**

a) Eleza majanga yanayozungumziwa katika taarifa hii.

b) Ni dalili zipi zinazoweza kukusaidia kumtambua mtu mwenye virusi vya Korona? Fafanua kwa mujibu taarifa hii.

c) Kulingana na taarifa hii, janga la korona liliathiri vipi watu wa jamii yako.

d) Fikiria kama wewe ni mhudumu wa afya, unaweza kuwasaidia vipi watu jamii kutoathirika kutokana na ugonjwa wa virusi vya Korona? Eleza.

e) Unaposoma taarifa hii, unajifunza njia zipi za kujilinda dhidi ya ugonjwa huu wa UVIKO19?

## SEHEMU B: FASIHI

**2. Soma dondoo hili na ujibu maswali yanayofuata hapo chini;**

**Mtanganzaji :** Hrrrrrrr….chaa! *( vigelegele na vifijo)*
Utamu ulioje huo! Sikia mziki! Penzi ni kulinda chozi…..wewe!
Disko hiyo kaiweke kwa bwana na Bi harusi. Msiharibu muziki
kabla ya wakati wake. Hebu leta mwingine unaofaa wageni tu,
au Sivyo?
One! Two! Three! Kibaooo.

**Bendi :** *Nakupenda kama mbuzi, apendavyo kula nyasi,*
*Hata kama huulizi Nakupenda bila wasiwasi.*

**Mtangazaji:** Kila kibao ni moto moto, kama mwanamziki maarufu Pepekale amefika! Vibao hivyo navitaka bwana na Bi harusi watakapofika. Hivyo ni vibao kweli kweli. Wakati wowote wataingia.Wakija,sote tuwafurahie tuwawonyeshe furaha na mapenzi.

*(Anaingia Kwatampola na wajenzi wengine)*

**Mtangazaji**: (Mtangazaji anatuliza makeke) mabibi na mabwana, tunaendelea kuwapokea wageni. Hao ambao wameingia sasa ni kina Kwatampola Waelekeze wakakae.Wapeni nafasi huko nyuma. Nafasi za mbele ni za wateule na wengi hawajafika. Viti vya mbele vihifadhiwe tafadhali.

*(Kwatampola na kikundi chake wanapewa nafasi nyuma)*

**Mjenzi 2:** Niliwaambia kuwa matajiri si watu. Ona sehemu ambayo tumewekwa. Tena mwenyewe alitualika; mjinga huyu anasema si wageni waalikwa.

**Mjenzi 1:** (*Akimkonyezea*) Sshhii! Chunga sana usije ukasikika.Wakatudhania wahuni. *(Anaingia Bumaali na mkewe wa kwanza,Bi Akello)*

**Mtangazaji:** Yo! Yo! Yo! Yo! Wewe! Ndiye mwenyewe aja! Pole! Pole! Pole! Makofi jamani makofi!

**Bumaali**: (*Kwa tabasamu*) Ahsanteni jamani. Mimi na mke wangu wa kwanza tumefurahi.(*wanachukua viti katika nafasi zao*) Asanteni sana!

**(vifijo)**

**Mtangazaji:** wawa waaaa! Ni huyu kabaila Bumaali. Kwa muda usio wa mbali sana tutampokea Bi harusi Maculate sherehe ianze. Atakapofika, tutapata kibao kutoka kwa wanamziki. Kisha tutakuwa na hotuba kutoka kwa bwana harusi akimkaribisha Bi harusi mpya pamoja na kutukaribisha sisi pia. *(Anaingia Bi harusi na jamaa zake. Vifijo na nderemo. Bumaali na Bi Akello wanasimama kumlaki)*

**Mtangazaji:** Hauchi hauchi unakucha! Hayawi hayawi yanakuwa! Wewe! Wanamuziki, One! Two! Three! Ngoma!

**Maswali;**

a) Dondoo hili linahusu nini?

b) Mhusika Bumaali anadhihirisha wasifu gani katika dondoo? Eleza.

c) Eleza maudhui yanayotiliwa nguvu katika dondoo hili.

d) Changanua mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili.

e) Unapata hisia zipi unaposoma dondoo hili? Tetetea jibu lako.

**MWISHO!**